

UVUMBUZI

1. Sasa ninatakadimu, niseme yanayong'aa,
Nimuambie mwalimu, aone kama yafaa,
Nae awape elimu, watoto wanaofaa,
Aliyevumbua saa, kaufaa ulimwengu
2. Zamani za kina babu, saa hazikuzagaa,
Ilikuwa ni sulubu, kujua siku na saa,
Leo hapanazo tabu, za kusali na kukaa,
Aliyevumbua saa , kaufaa ulimwengu.
3. Safari walipotaka, mizigo walijitwaa,
Nyumbani wakaondoka, safari wakashikaa,
Abusa zikawafika, wengine kutawafaa,
Alounda motakaa, kaufaa ulimwengu.
4. Leo tunaposafiri, tabu zinatuaambaa,
Hatuzipati hatari, kabula ya kufikaa,
Maili sabutashari, hazitimu hata saa,
Alounda motakaa, kaufaa ulimwengu.
5. Ilikuwa ni vigumu, kwa watu waliokaa,
Kigoma au Kisumu, habari kuzitandaa,
Leo ai! Si hamumu, mambo mengi yanapaa,
Alovumbua radio, kaufaa ulimwengu.
6. Hata uharabu pia, nao pia una taa,
Mabomu wamevumbua, kuua yanayofaa,
Leo tunajiombea, tusigeuzwe mkaa,
Alogundua mabomu, kaudhuru ulimwengu.
7. Mengine twaona pia, mazuri yanayofaa,
Mashine za kuchapia, zingine za kutwangaa,
Ndege na treni pia, vingi vilotapakaa,
Ugunduzi waloanza, wamefaa ulimwengu.
8. Tamati na nitulie, sasa bora kunyamaa,
Wengine niwaachie, kama alounda taa,
Wazuri wajitambue, ulimwengu wamefaa,
Ugunduzi waloanza, wamefaa ulimwengu.

Hamidu R. Tambwe